



## **AZIMIO NA. 07 /2017**

### **AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA AMANI NA USALAMA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (*THE EAST AFRICAN COMMUNITY PROTOCOL ON PEACE AND SECURITY*)**

**KWA KUWA,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community – EAC*) kwa mujibu wa Ibara ya 3(1) ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao ulisainiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama wa *EAC* uliofanyika mjini Arusha, tarehe 30 Novemba, 1990;

**NA KWA KUWA,** Ibara ya 151 ya Mkataba huo ya Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 1999 (*The Treaty for the Establishment of the East African Community*) inatoa Mamalaka kwa nchi wanachama kuandaa na kuridhia Itifaki katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Jumuiya;

**NA KWA KUWA,** Mkataba huo Unaelekeza kwamba kila Itifaki itakayoandaliwa itaidhinsihwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itakuwa wazi kwa ajili ya kusainiwa na hatimaye kuridhiwa na Nchi Wanachama kwa mujibu wa taratibu zao;

**NA KWA KUWA,** Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*) iliidhinishwa na Mkutano wa 14 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa *EAC* uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2012 Mjini Nairobi Kenya na kusainiwa na Mawaziri kutoka nchi wanachama wa Jumuiya tarehe 15 Februari, 2013 ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mojawapo ya Nchi Wanachama wa *EAC* iliyosaini Itifaki hii;

**NA KWA KUWA**, lengo la Itifaki hii, ni kuimarisha amani, usalama na utulivu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kukuza ujirani mwema kwa nchi wanachama;

**NA KWA KUWA**, kwa kujiunga na Itifaki hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaimarisha ushirikiano wake na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kutatua migogoro mbalimbali katika Jumuiya na hivyo kuimarisha ujirani mwema, kuwepo na amani na usalama kutokana na kubadilishana taarifa za uhalifu na uhalifu unaovuka mipaka, kupata taarifa za kuibuka kwa makosa mapya, kuimarisha mapambano dhidi ya ugaidi, dawa za kulevya, biashara haramu ya binadamu, kuenea kwa silaha haramu ndogo ndogo na nyepesi, wizi wa mtandaoni na vilevile kusaidia katika kubadilishana ujuzi na uzoefu katika kukabiliana na uhalifu;

**HIVYO BASI**, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii kwa Tanzania na pia umuhimu wa kuridhia Itifaki hii, Bunge hili katika Mkutano wa Nane na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka, 1977 linaazimia kuridhia Itifaki hii iitwayo **ITIFAKI YA AMANI NA USALAMA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (THE EAST AFRICAN COMMUNITY PROTOCOL ON PEACE AND SECURITY)**.

**Limepitishwa na Bunge leo tarehe 7 Septemba, 2017.**

Dkt. Thomas D. Kasilillah  
**KATIBU WA BUNGE**